The Guardian
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
TANZANIA WEDNESDAY 29 SEPTEMBER, 2021

National Pg 3
Diaspora urged to invest in Tanzania



National Pg 4
Revamping the tourism sector



National Pg 6
Services for persons with disabilities





Page 13

# Samia takes census, vaccines appeal to church anniversary



# State in grief after Ole Nasha's death



# Govt handed fish farm plan for Lake Victoria

"Therefore you can see our efforts have resulted in having big investors in the sector, including Tengreen"

# Ziwa Victoria kufanyiwa mpango bora wa matumizi kukuza uchumi

**Na Mbaraka Kambona, Mwanza**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imejipanga kufanya mpango wa matumizi bora ya ziwa Victoria ambao utaainisha maeneo ambayo yatatumika kufanya ufugaji wa vizimba ili kutoa nafasi pia kwa shughuli za uvuvi wa asili kuendelea bila kuwa na muingiliano.

Ulega aliyasema hayo juzi alipotembelea eneo la Kampuni ya Kichina ya Tangreen iliyowekeza katika mradi wa ufugaji wa Samaki kwa kutumia vizimba kandokando ya ziwa Victoria, jijini Mwanza.

Alisema kuwa serikali imedhamiria kufanya hivyo ili kupunguza muingiliano wa shughuli za ufugaji wa Samaki na Uvuvi wa asili ili shughuli zote zifanyike kwa ufanisi na kuleta tija katika uchumi wa buluu.

"Mpango wa Serikali ni kuhakikisha ufugaji wa vizimba unafanyika katika maeneo maalum na sio kila mahala, tuwe na maeneo mahususi ya kazi hii ili kutoa nafasi pia wavuvi wa asili waweze kuendelea na shughuli zao," alisema Ulega.

Waziri Ulega alisema kuwa mpango huo pia utavutia wawekezaji wengi kuwekeza katika ziwa Victoria, na wao kama Serikali wanawakaribisha wawekezaji kama TanGreen kuja kuwekeza nchini.

"Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji, na hivi karibuni tumemuona akifanya jitihada kubwa kwa kutangaza nchi yetu katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kufungua milango ya uwekezaji, na moja ya maeneo ya uwekezaji aliyokuwa akiyatangaza ni katika uchumi wa buluu," alisema Ulega.

Aliongeza kuwa TanGreen imejikita katika kukuza uchumi wa buluu kwa kufuga Samaki wa vizimba na wanatarajia kuvuna Tani Elfu kumi (10, 0000) kwa mwaka, huku akisema kuwa kwa sasa nchini samaki wanaovuliwa kutoka kwenye mabwawa ni Tani Elfu Ishirini na Mbili (22,000) hivyo TanGreen wanakwenda kuzalisha nusu ya kile kinachozalishwa sasa nchini.

Aidha, aimuelekeza Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salim Mkali kuhakikisha muwekezaji huyo analindwa, na kama kutakuwa na wadokozi wenye nia ya kurudisha nyuma kampuni hiyo wawachukulie hatua kali.

Ulega aliendelea kusema kuwa bado kunahitajika kubwa la Samaki nchini, kiasi kinachohitajika kwa mwaka ni Tani Laki Saba (700, 000) wakati uwezo uliopo kwa sasa ni kuzalisha Tani Laki Nne (400, 000) hivyo kufanya upungufu ya Tani Laki Tatu (300,000) huku akisema ufugaji wa vizimba ukifanyika vizuri utasaidia kupunguza changamoto hiyo nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Ruhumbi alisema kuwa wamejipanga kufanya Mkoa huo kuwa mzalishaji mkubwa wa Samaki wa kufugwa katika mabwawa.

Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah alisema kuwa Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wameendelea kuhamasisha uwekezaji wa mitaji na wamehamasisha mabenki kama Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na imeshaanza kutoa mikopo, huku akisema wanaendelea kuwashawishi wawekeza wakubwa wa mitaji kuwekeza katika ufugaji wa samaki na kukuza uchumi wa buluu.

"Hivyo unaweza kuona kuwa ushawishi tulioufanya ndio umepelekea wawekezaji wakubwa kama TanGreen kujitokeza na kwa kweli imeleta tija kwa sababu miaka mitatu iliyopita tulikuwa na vizimba 18, lakini kwa sasa tuna vizimba 473 na asilimia 77 ya vizimba vyote vipo hapa ziwa Victoria," alisema Dkt. Tamatamah.

Awali, Daktari wa Samaki wa Kampuni ya TanGreen, Dkt. Mugure Katwiga Marwanda akisoma taarifa fupi ya Kwanda hicho alisema kuwa moja ya lengo la Kampuni hiyo ni kukuza na kutangaza teknolojia ya ufugaji ikiwemo kufungua fursa ya ajira kwa vijana.

"Naibu Waziri, pamoja na jitihada tunazoendelea nazo lakini tunakumbana na changamoto kadhaa ikiwemo uhaba wa vifaranga vya Samaki ndani ya nchi, baadhi ya wavuvi kuingia ndani ya mradi kuiba au kuharibu miundombinu," alisema Dkt. Katwiga Marwanda.

Aliongeza kwa kuiomba Serikali itoe vibali vya kuingiza vifaranga vya samaki kutoka nje ya nchi ili kukidhi mahitaji yaliyopo huku akiiomba Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii ya wavuvi juu ya uwekezaji wa vizimba ili waache kufanya shughuli za uvuvi katika mradi huo.

## Mbegu bora za kilimo zaanza kusambazwa kwa wakulima

**Na Allan Vicent, Morogoro**

WAKALA wa mbegu za kilimo nchini (ASA) wameanza kusambaza mbegu bora kwa wakulima kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa kilimo wa 2021/2022 ili kuwarahisishia upatikanaji wake.

Mbegu hizo zimeanza kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini kwa kutumia

UK 7.

# Maelfu wang'atwa na mbwa wenye kichaa

**Magnus Mahenge, Dodoma**

KATI ya Januari hadi Agosti mwaka huu watu 39,787 wameripotiwa kung'atwa na mbwa au wanyama jamii hiyo wenye kichaa (kichaa cha mbwa) nchini.

Takwimu hizo zilitolewa na Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Dk James Kihologwe kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Abel Makubi.

Akizungumzia Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani iliyoadhimishwa jana Dk Kihologwe alisema kwa Tanzania ugonjwa wa kichaa cha mbwa uliripotiwa kwa mara ya kwanza 1932, na tangu hapo umeendelea kuripotiwa katika maeneo mbalimbali na kwa kiwango tofauti.

Kati ya takwimu hizo, alisema mikoa ya Morogoro unongoza kwa na watu 4,329 waliong'atwa na mbwa na mkoa wa Dodoma ni wa pili kwa kuwa na watu 4,233.

Profesa Makubi alisema tatizo la kichaa cha mbwa ni kubwa kuliko inavyofikirika, kwani takwimu hizo hazijumuishi matukio yaliyotokea katika vituo vya kutolea huduma bila kutolewa taarifa au yaliyotokea nyumbani na waathirika ambao hawajafika katika vituo vya kutolea huduma.

Utafiti uliofanyika mwaka 2002 ulibainisha kuwepo na uwezekano wa takribani vifo 1,499 kwa mwaka vinavyotokana ma ugonjwa huo.

Makubi alisema waathirika wakubwa wa ugonjwa huo ni watoto chini ya miaka 15 kutokana na ukweli kwamba ndio wanakuwa karibu na mbwa wanaofugwa na pia hupenda kucheza au kuchokoza mbwa wasiowafahamu njiani.

"Pamoja na ugonjwa huu kusababisha vifo, pia husababisha athari za kiuchumi kutokana na chanjo zake kuuzwa kwa gharama kubwa," alisema.

Katika kudhibiti ugonjwa huo, Wizara ya Afya imeshirikiana na sekta nyingine ikiwemo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Waziri Mkuu (dawati la afya moja), wadau mbalimbali pamoja na Shirika la Afya Duniani, Shirika la Chakula Duniani na wengine katika kupunguza ukubwa wa tatizo linalohusiana na ugonjwa huo.

Katika kufanikisha hilo, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma, kuboresha dhana ya afya moja nchini, kurahisha upatikanaji wa huduma ya chanjo ya kichaa cha mbwa kwa wananchi pamoja na kurahisisha upatikanaji wa huduma ya chanjo kwa wanyama hasa mpya.

Ugonjwa huu hutoka kwa mnyama jamii ya mbwa aliyeathirika na virusi vya kichaa cha mbwa ikiwemo paka, mbweha na fisi na binadamu huupata kwa kung'atwa na wanyama hao.

Kama mtu aking'atwa na mbwa, ni budi kuosha jereha kwa dakika 10 au zaidi kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni halafu kidonda kisifungwe.

**"Pamoja na ugonjwa huu kusababisha vifo, pia husababisha athari za kiuchumi kutokana na chanjo zake kuuzwa kwa gharama kubwa," alisema.**



# TEF yapongeza viongozi serikalini kutoa taarifa

**Na Aveline Kitomary**

... utembee sana. Ukifika ukakutane na mlinzi, katibu kwa hiyo vikwazo mpaka ...

fursa iliyojitokeza. Maana yangu ni kwamba kuna upotoshaji mwingi sana mfano wakati wa chanjo ya corona ...